SIGNATURE: ..........DATE: ..............
DESIGNATION: COMMISSIONER FOR OATHS

karibu naye au awasiliane naye ka simu Na. –

KILOMBERO IFAKARA

simu Na. 0747176896.

UHURU UK 20

# Ulega akabidhi misaada kwa waathirika Hanang

**Na Mwandishi Wetu,** *Hanang*

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amekabidhi misaada iliyotolewa na wadau wa sekta ya mifugo kwa waathirika wa maafa ya maporomoko ya mawe wilayani Hanang, mkoani Manyara.

Miongoni mwa vitu viliyokabidhiwa ni ng'ombe 13, Mbuzi 20, trei za mayai 90, fedha tasilimu sh. milioni tano, katoni 300 za maziwa, unga wa sembe, maharage na chumvi.

Msaada huo ulikabidhiwa jana kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama kwa niaba ya waathirika wa mafuriko hayo.

Waziri Ulega alikabidhi misaada hiyo wilayani humo, alipofika kwa lengo la kutoa mkono wa pole kwa waathirika wa maafa hayo yaliyoharibu miundombinu na kusababisha vifo.

Akitoa salamu za wizara, Waziri Ulega alisema wamepokea kwa masikitiko makubwa tukio la mafuriko hayo yaliyotokea na kusababisha kupotea kwa maisha ya Watanzania na uharibifu wa mali na mifugo.

"Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Asas, Bajuta International, Dalberg International, Karie Kinana, Apoka, Tafma Afma, Tabrofa na TPBA, tumeandaa vitu na kuvikabidhi kwa Kamati ya Maafa ya Kitaifa itakayoratibu namna nzuri ya kuvifikisha kwa familia na walengwa.

"Tunaungana na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kutoa pole kwa familia zilizokumbwa na maafa haya yaliyoumiza mioyo ya Watanzania wote. Tutashirikiana na Kamati ya Taifa ya Maafa na uongozi wa mkoa na wilaya kubaini uharibifu wa miundombinu ya mifugo na kuirejesha katika hali yake ya kawaida," alisema.

Waziri Ulega aliendelea kusisitiza serikali chini ya Rais Samia itaendelea kusimama na Watanzania wote katika hali zote zinazowapata kuhakikisha azma ya mkuu huyo wa nchi ya kuwaletea maendeleo inatimia.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga alitoa shukrani kwa wadau wanaoendelea kujitokeza kuwafariji katika kipindi hiki kigumu.

CamScanner

wakiteseka na wengi
wakishindwa kugharamia

kwa kila mgonjwa
dialysis ni Sh 300,0

HABARI LEO UK 4

# Ulega akabidhi ng'ombe, mbuzi, mayai, fedha waathirika Hanang

**Na Mwandishi Maalumu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amekabidhi misaada vikiwemo vyakula vya mifugo kwa waathirika wa maafa ya maporomoko ya tope wilayani Hanang mkoani Manyara.

Miongoni mwa vitu vilivyokabidhiwa ni pamoja na ng'ombe 13, mbuzi 20, trei 90 za mayai, fedha taslimu Sh milioni tano, katoni 300 za maziwa, unga wa sembe, maharage na chumvi.

Msaada huo ulikabidhiwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama kwa niaba ya waathirika wa mafuriko hayo.

Misaada hiyo ilitolewa na wadau wa sekta ya mifugo na ilikabidhiwa na Ulega aliyefika Hanang kutoa mkono wa pole kwa waathirika wa maafa hayo.

"Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo Asas, Bajuta International, Dalberg International, Karie Kinana, Apoka, Tafma Afma, Tabrofa na TPBA, tumeandaa vitu na kuvikabidhi kwa Kamati ya Maafa ya Kitaifa itakayoratibu namna nzuri ya kuvifikisha kwa familia na walengwa," alisema Ulega.

Aliongeza: "Tunaungana na Rais Samia kutoa pole kwa familia zote zilizokumbwa na maafa haya yaliyoumiza mioyo ya Watanzania wote.

"Tutashirikiana na Kamati ya Taifa ya Maafa na uongozi wa mkoa na wilaya ili kubaini uharibifu wa miundombinu ya mifugo na kuirejesha katika hali yake ya kawaida."

Ulega alisema serikali itaendelea kuwa na Watanzania katika hali zote zinazowapata.

# Samaki wapandikizwa katika bwawa la mgodi lililobomoka

Na Marco Maduhu,
KISHAPU

BWAWA jipya la Mwang'olo lililojengwa na mgodi wa madini ya almasi (WDL) wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga limepandikizwa vifaranga 5,000 vya samaki aina ya sato ikiwa ni sehemu ya kurejesha hali ya awali ya bwawa lililobomoka kingo zake mwishoni mwa mwaka jana.

Awali bwawa lililobomoka lilikuwa na mazalia ya samaki, waliowasaidia wakazi wa maeneo hayo kujishughulisha na uvuvi. Mgodi huo umeamua kupandikiza samaki wengine ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali la kurudisha bwawa hilo katika hali yake ya awali.

Meneja Uhusiano mgodi huo, Bernard Mihayo, akizungumza wakati wa upandikizaji huo, alisema agizo la serikali ni kurudisha kila kitu ambacho kiliharibika baada ya kupasuka kwa bwawa la majitope la mgodi wao Novemba mwaka jana na kuleta madhara kwa wananchi.

"Tayari tumekamilisha ulipaji fidia kwa waathirika. Tunachokifanya sasa ni kuhakikisha tunarudisha hali ya mazingira kama ilivyokuwa awali ikiwa ni pamoja na kupanda miti.

"Vilevile, tunapandikiza vifaranga hawa ili wananchi waendelee na shughuli zao kama kawaida ikiwamo uvuvi wa samaki na kuinuka kiuchumi na kupata kitoweo kama ilivyokuwa awali," alisema Mihayo.

Alitaja vifaranga 5,000 vimepandikizwa... Katika kuhifadhi mazingira ya eneo hilo, tayari wamepanda miti 10,000 na upandaji miti utakuwa endelevu kuhakikisha eneo hilo linarejea katika asili yake.

Ofisa Uvuvi Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Moses Ng'winza, aliwataka wakazi wa eneo hilo kusubiri hadi miezi sita ipite ndipo samaki hao wawe tayari kwa shughuli za uvuvi. Serikali itatoa elimu na maelekezo kuhusu uvuvi katika eneo hilo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kishapu, Fatma Mohamed, aliwata wananchi kuendelea kulitunza bwawa hilo na kila mmoja awe mlinzi wa mwezake, pia akikemea kilimo karibu na bwawa hilo.

CamScanner